

Orodha wa ugonjwa wa virusi vipya vya korona ya 2019 (COVID-19)

Imesasishwa: 4/4/2020

Ugonjwa wa virusi mpya vya korona ya 2019 (COVID-19) ni aina mpya ya virusi vya korona iliyogunduliwa kwanza katika China na imegunduliwa sasa katika nchi nyingi, ikiwa ni pamoja na Marekani na katika Iowa.

Kuna virusi saba vya virusi vya korona vinavyojulikana kuwaambukiza binadamu, ikiwa ni pamoja na nne vya kawaida sana, kali kidogo vinavyosababisha ugonjwa sawa na mafua ya kawaida. Watoa huduma ya afya wanapima virusi hivi vya kawaida vya korona mara kwa mara na hakuna harakati za afya ya ummazinazohitajika kukabiliana na virusi hivi vya kawaida vya korona. Tatu ya virusi hivyo saba vya korona ni nadra na vinaweza kusababisha ugonjwa kali zaidi, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa virusi mpya vya korona ya 2019 (COVID-19).

Dalili:

Dalili zinaweza kuonekana siku 2-14 baada ya kashifa na zinaweza kuwa ni pamoja na:

- Homa
- Kikohozi
- Upungufu wa pumzi

Magonjwa yaliyoripotiwa ni mbalimbali kuanzia na watu kuwa wagonjwa kwa kiwango cha chini hadi watu kuwa wagonjwa zaidi na kufa. Wagonjwa wazee na wale walio na matatizo mahututi ya kiafya Huenda wakawa hatarini zaidi kwa ugonjwa mkali.

Kwa sasa hakuna tiba maalumu ya COVID-19. Watu walio na COVID-19 wanapokea utunzaji wa utegemeo wa kuasaidia kupunguza dalili.

Kupima:

Upimaji zaidi umeanza kupatikana kila siku kupitia Maabara ya Usafi ya Nchi (SHL) na kupiti maabara ya kibinafsi. Mtoaji wako wa huduma ya afya atatathmini kama unahitaji kupimwa, na anaweza kushauriana na afya ya umma wakiuliza maswali. Uongozi wa upimaji unapatikana hapa: <http://shl.uiowa.edu/dcd/covid19.xml>

Rasilimali za ziada za upimaji zinapatikana hapa: <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/symptoms-testing/testing.html>

Uenezaji:

Virusi vinasambazawa haswa kutoka kwa mtu-kwa-mtu kati ya watu walio katika mawasiliano ya karibu (kama futi sita hivi). Uenezaji hutokea kutokana na tone za kupumua zinazozalishwa wakati mtu aliyeambukizwa anakohoa au kupiga chafya na zinazoangukia midomo au mapua ya watu walio karibu au labda pia zinapumuliwa mapafuni. Kuna uwezekano kupata COVID-19 kwa kugusa eneo au kitu kilicho na virusi kisha kugusa mdomo wako, pua, au macho, lakini hii haijafikiriwa kuwa njia kuu ambayo virusi vinaenea.

Uzuiaji:

Jifunzeni kutokaribiana. Kutokaribiana ni kuwa na futi 6 au zaidi kati yaw ewe and watu waisoishi nyumbani kwako. Kama huwezehimili kutokaribiana, jaribu uwe unavaa barakoa.

Kwa kuongeza, CDC inajulisha IDPH wasafiri wagonjwa wanaokuja kutoka China na Iran (Wasafiri wagonjwa watahudumiwa na wahudumu wa afya kabla ya kuachiliwa kutoka uwanja wa ndege). Afya ya umma ndipo itachunguza hawa wagonjwa wana magonjwa kiasi gani na maagizo ya ukaguzi wa afya ya umma ambayo yaelezea mahitaji ya kuripoti dalili kwa afya ya umma mara mbili kwa siku vizuizi kwa shughuli za kila siku

Watu waliomaliza utengaji wao wa kijamii wa siku 14 au ufuatiliaji wa afya ya umma hawako hatarini kusambaza COVID-19.

Kwa sasa hakuna chanjo ya kuzuia ugonjwa wa 2019 wa virusi vya korona (COVID-19). Njia bora ya kuzuia ugonjwa ni kuepuka kujikashifu kwa virusi hivi. Watu wanaweza kusaidia kuzuia kuenea kwa magonjwa ya kupumua kwa wengine kwa kufunika vikohozi na chafya zao, kusafisha mikono yao mara kwa mara, na kukaa nyumbani wakiwa mgonjwa.

Taarifa ya Uwasiliano

Idara ya Iowa ya Afya ya Umma

Tafadhali piga simu kwa 211 kwa ajili
ya maswali ya jumla
(800) 362-2736